**AFRICA INLAND CHURCH TANZANIA**
**DAYOSISI YA SHINYANGA**
**OFISI YA ASKOFU S.L.P. 53 SHINYANGA, TANZANIA**
**Bishops' Office: Zion Street, Old Shinyanga Road, Lubaga Barua pepe: aictshyadmn@gmail.com**

# TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Kanisa la **Africa Inland Church Tanzania (AICT) Dayosisi ya Shinyanga** limekuwa likitoa huduma kwa watoto wanaotoka kwenye kaya maskini kupitia kituo cha Huduma ya maendeleo kamilifu ya Mtoto (Holistic Child Development Ministry) kwa kushirikiana na Shirika la Compassion International Tanzania (CIT). Kanisa kupitia Program za maendeleo kamilifu ya mtoto linalenga kuwafungua watoto katika umaskini kwenye maeneo ya Kiroho, Kiuchumi, Kijamii na Kimwili (ambao ndio ujumla wa mtu), kwa shabaha ya kuwawezesha wawe watu wazima wanaojua wajibu wao na wanaojitosheleza.

## UTUMISHI WA WATENDA KAZI VITUO VYA HUDUMA YA MTOTO NA KIJANA KANISA LA AICT DAYOSISI YA SHINYANGA

Watumishi wote wa Vituo vya Huduma ya Mtoto na Kijana ni waajiriwa wa kanisa la AICT kupitia Ofisi ya Katibu wa Dayosisi hivyo **atawajibika kwa Katibu wa Dayosisi ya Shinyanga**, na kusimamiwa moja kwa moja na Mchungaji Kiongozi (Kwa niaba ya Baraza la Local Church) na Kamati ya Huduma ya Mtoto, kwa mujibu wa Mwongozo wa Ajira ya Dayosisi na Huduma ya Mtoto kiujumla ya Compassion International Tanzania (CIT) katika Ushirikawenza na Makanisa ya Kiinjili Tanzania.

**Katibu wa Dayosisi AICT Dayosisi ya Shinyanga (Kwa niaba ya Baraza la Utendaji la AICT Dayosisi ya Shinyanga)**, anakaribisha maombi kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi zifuatazo:

1. **MRATIBU (NAFASI 1)**

<u>**SIFA ZA WAOMBAJI**</u>

i. Awe Mkristo aliyeokoka na kujitoa kwa Bwana Yesu; mwenye maisha ya Ushuhuda ya kila siku. Mwenye moyo wa kujitoa, kutumika kanisani na mpenda maendeleo, anayependa kufanya kazi na Watoto na Vijana kutoka katika mazingira magumu.
ii. Awe tayari kushiriki ibada za kanisa la AICT kipindi cha utumishi wake ili aweze kuwavuta walengwa waje kwa Yesu.
iii. Awe na elimu ya ngazi ya Stashahada **(Diploma)** au Shahada ya kwanza **(Digrii)** na kuendelea katika maswala ya Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii, Sosholojia, Usimamizi wa Miradi, Uongozi & Utawala, Usimamizi wa rasilimali watu.
iv. Awe na uzoefu usiopungua miaka 3 katika kufanyakazi au kusimamia miradi.
v. Awe na moyo wa kuwapenda watoto, na kutumika kanisani.
vi. Awe na uwezo wa kuongea, kusoma, na kuandika kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili kwa ufasaha.
vii. Asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa la unyanyasaji wa mtoto.
viii. Awe na uwezo na elimu ya kutumia kompyuta hasa programu kama 'Micro-soft office' (Word, Excel, Power Point) na Email.
ix. Awe na uzoefu katika uandishi na usimamizi wa Miradi ya Maendeleo.
x. Awe na umri kuanzia miaka 25 na asizidi miaka 45.

**Kazi na majukumu ya Mhasibu wa kituo Cha Maendeleo ya Mtoto na Kijana**

i. Kuandaa mpango na bajeti ya huduma yam toto kwa kushirikiana na watendakazi wengine wa huduma yam toto na kuwasilisha kwa kamati ya huduma ya mtoto kwa uthibitisho na kuidhinishwa na uongozi wa kanisa.
ii. Kutekeleza mpango na bajeti ya programu kama ilivyothibitishwa na kuidhinishwa.
iii. Kusimamia na kuratibu shughuli zote za wafanyakazi wengine wa kituo cha huduma yam toto.
iv. Kuwasilisha ripoti kwa kamati/uongozi wa kanisa na huduma ya Compassion international Tanzania kama itakavyotakiwa na pande zote husika.

v. Kuhakikisha taarifa zote za Watoto na fedha zinatunzwa na kupatikana wakati wote zitakapohitajika.
vi. Kusimamia maono na vithaminisho vyote vya huduma na misingi ya huduma wakati wote wa uhai wa kituo cha huduma yam toto.
vii. Kushiriki katika zoezi la usaili la kuwapata watendakazi wengine wa kituo cha huduma yam toto kwa kutoa maoni kuhusu nafsi hizo.
viii. Kuhakikisha mazingira ya Watoto au vijana kituoni ni slaama kwao kujifunza na kushiriki katika programu zote za kituoni.
ix. Atasimamia na kuwa mwangalizi mkuu wa utekelezaji wa mitaala yote inayotumika kituoni ,msimamizi wa shughuli zote za ufundishwaji na usimamizi wa waalimu wote.
x. Atawajibika kuandaa na kuandika maandiko mbalimbali Proposal kwa ajili ya mahitaji mbalimbali ya Watoto na wazazi na kituo kwa ujumla.
xi. Kuhakikisha uwepo wa miundombinu inayohitajika kwa wtoto au vijana inapatikana.
xii. Uhamasishaji wa rasilimali zilizopo na kutafuta njia mbadala na pukata miundombinu kwa ajili ya Watoto au vijana.
xiii. Kuhakikisha ripoti zote za kituo za utendaji zinaandaliwa na kuwasilishwa kwa wakati na ubora unatakiwa au unaotegemewa.
xiv. Kutathimini maendeleo ya watendakazi wengine wa huduma yam toto na kuwasilisha maoni yake kwa kamati ya huduma yam toto.
xv. \kufatilia kwa karibu manendeleo ya kiroho,Kijamii, elimu, Kiafaya na maswala mengine kwa Watoto yaliyopo kwenye programu na kuyachukulia hatua ya karaka pale inapobidi na kuwatembelea majumbani mwao.
xvi. Atawajibika kwa matokeo yote tarajiwa KRIs (Key Results Indicators) matokeo ya ukaguzi kulingana na PFM.
xvii. Kuhakikisha kwamba Watoto wameandika barua kwa wafadhili wao kwa wakati muafaka, kwa kiwango kinachotakiwa na kwa mujibu wa programu.
xviii. Kuhakikisha zawadi za Watoto zilizotumwa zinawafikia walengwa kwa wakati muafaka na kwa kiwango kinachopaswa.
xix. Kushiriki katika mafunzo ya kiroho yaliyoandaliwa na Compassion katika huduma yam toto kwa ujumla
xx. Kupitisha gharama zote za malipo sambamba na maelekezo yaliyotolewa na kamati ya huduma ya mtoto na pia kulingana na miongozo ya kifedha ya Compassion International.
xxi. Kuwasidia watendakazi wengine na kushirikiana pale inapohitajika.
xxii. Kuwatembelea Watoto wajumbani na mashuleni sambamba na programu na mpango wa huduma yam toto.
xxiii. Kutoa taarifa kwa kamati ya huduma ya mtoto/mchungaji kiongozi na katika ofisi husika juu ya ubadhilifu wa fedha au tabia mbaya kwa wafanyakazi wengine inapojitokeza.
xxiv. Kushiriki katika shughuli zote za barua za Watoto zinazoingia na zinazotoka.
xxv. Kutunza kitabu cha hundi na kitabu cha hati ya malipo.
xxvi. Kuhakikisha wakati wote kwamba watoto wote walioandikishwa katika huduma yam toto katika ufadhili ni wale tu waliokidhi vigezo vya Compassion Internationa Tanzania.
xxvii. Kuwatia moyo wazazi na walezi kuwasaidia Watoto kuweza kukua kiroho na kuwa na maendeleo mazuri katika masomo.
xxviii. Kuhusika katika majukumu mengine yoyote yaliyotolewa na kamati ya huduma yam toto au Ofisi ya Dayosisi na Compassion International.
xxix. Kutoa taarifa juu ya utendaji na maendeleo ya kituo kwa mamalaka zinazotakiwa.
xxx. Atawajibika kwa kamati na mchungaji kiongozi.
xxxi. Atahakikisha kunakuwa na ibada ya asubuhi ya watendakazi wote kabla ya kuanza kazi na kushiriki ibada hiyo kikamilifu.
xxxii. Ataitisha na kuratibu vikao vya wazazi kwa kushirikiana na mweyekiti wa kamati ya wazazi.
xxxiii. Ataitisha na kuendesha vikao na watendakazi kila mwezi na pale itakapobidi.
xxxiv. Atatafsiri barua zote za Watoto zinazotoka kwa wafadhili.
xxxv. Atasimamia na kuratibu shughuli zote za mama wa ufadhili wa upendo (Esther Encounter).
xxxvi. Atafanyakazi nyinginezo kama atakavyopangiwa na kamati ya kituo cha huduma yam toto na uongozi wa kanisa.

**2. MHASIBU. (NAFASI 3)**

**SIFA ZA WAOMBAJI**

i. Awe Mkristo aliyeokoka na kujitoa kwa Bwana Yesu; mwenye maisha ya Ushuhuda ya kila siku. Mwenye moyo wa kujitoa, kutumika kanisani na mpenda maendeleo, anayependa kufanya kazi na Watoto na Vijana kutoka katika mazingira magumu.
ii. Awe tayari kushiriki ibada za kanisa la AICT kipindi cha utumishi wake ili aweze kuwavuta walengwa waje kwa Yesu.
iii. Awe na elimu ya ngazi ya Stashahada **(Diploma)** au Shahada ya kwanza (**Digrii**) na kuendelea katika fani ya Uhasibu, Fedha, Biashara na Usimamizi wa fedha.
iv. Awe na uzoefu usiopungua miaka 3 katika fani ya Uhasibu.
v. Awe na uwezo wa kutumia mifumo ya kihasibu ***(Accounting software packages mfano Quickbooks na nyinginezo)***
vi. Awe na moyo wa kuwapenda watoto, na kutumika kanisani.
vii. Awe na uwezo wa kuongea, kusoma, na kuandika kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili kwa ufasaha.
viii. Asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa la unyanyasaji wa mtoto.
ix. Awe na uwezo na elimu ya kutumia kompyuta hasa programu kama 'Micro-soft office' (Word, Excel, Power Point) na Email.
x. Awe na uzoefu katika uandishi na usimamizi wa Miradi ya Maendeleo.
xi. Awe na umri kuanzia miaka 25 na asizidi miaka 45.

**Kazi na majukumu ya Mhasibu wa kituo Cha Maendeleo ya Mtoto na Kijana**

i. Atamshuhudia Yesu Kristo kwa uaminifu na kuwa mtetezi wa watoto na vijana.
ii. Kuhakikisha kuwa vitabu vyote vya mahesabu vinatunzwa vizuri katika hali bora na ya usalama.
iii. Kuandaa na kutoa hundi zote za malipo kwa utaratibu uliowekwa.
iv. Kuhakikisha kuwa maagizo yote yatokanayo na risiti/stakabadhi mbalimbali za fedha pamoja na viambatanisho vyake vinaratibiwa vizuri kila wakati.
v. Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya matumizi ya fedha za huduma za mtoto kila mwezi kupitia kwa mratibu Kwenda kwa kamati ya huduma ya mtoto,uongozi wa kanisa na hatimaye ofisi za compassion international Tanzania.
vi. Kutoa malipo kutokana na uamuzi wa kamati na mratibu wa huduma yam toto kama ilivyopangwa na kwa mujibu wa sera na kanuni za kifedha za Compassion International Tanzania.
vii. Kuweka na kutunza fedha za kituo katika akaunti maalum iliyofunguliwa katika benki husika kwa ajili ya shughuli za huduma ya Mtoto katika kituo.
viii. Kufanya malipo yote stahiki yahusuyo shughuli za Huduma ya Mtoto kwa mujibu wa bajeti ya kituo kwa kipindi husika kwa kuzingatia kanuni za fedha za AICT na Compassion Internation Tanzania.
ix. Kushiriki kuwatembelea watoto na vijana majumbani na shuleni ili kufuatilia maendeleo yao kulingana na PFM na kuchukua hatua stahiki.
x. Kuandaa ripoti ya kazi kwa kipindi husika na kisha kuiwasilisha kwa mratibu wa kituo cha huduma yam toto.
xi. Kuwatia moyo wazazi na walezi wa watoto na vijana na wajumbe wa kanisa kuwasaidia watoto na vijana kukua kiroho na kuwa na maendeleo ya mazuri kimasomo.
xii. Kuungana na watenda kazi wengine kuwa sehemu ya waalimu wa watoto/vijana siku za program
xiii. Kuandaa mpango kazi wa kila wiki na kila mwezi kisha kuiwasilisha kwa Mratibu wa Kituo.
xiv. Kuandaa taarifa ya utekelezaji ya wiki na ya mwezi kisha kuiwasilisha kwa Mratibu wa Kituo.
xv. Kushiriki vikao vyote halali vilivyopangwa na kituo cha Huduma ya Mtoto, Compassion Intrernational na Kanisa la AICT.
xvi. Kutoa taarifa kwa kamati ya huduma ya mtoto, mchungaji kiongozi na katika ofisi za Compassion International Tanzania juu ya ubadhilifu wa fedha pale unapojitokeza.
xvii. Kushirikiana na watenda kazi wengine wa Kituo, Mchungaji wa Kanisa la Mtaa na Kamati ya Huduma ya Mtoto katika kutatu changamoto zote zitakazojitokeza katika utendaji kazi wa siku kwa siku.
xviii. Kuanda na taarifa ya fedha ya kituo za kila mwezi, robo mwaka, nusu mwaka na kuwasilisha katika ngazi za juu za kanisa la AICT (Dayosisi) na Compassion International Tanzania kwa kuzingatia miongozo ya fedha iliyopo na itakayowekwa.
xix. Atasimamia maono ya maendeleo ya ujumla ya mtoto na kijana na amali za huduma wakati wote wa Uhai wa kituo cha Huduma ya Mtoto.

xx. Kushirikana na watenda kazi wengine kuandaa mpango kazi na bajeti ya mwaka ya kituo cha maendeleo ya mtoto na kijana na kuwasilisha kwa Kamati ya Huduma ya Mtoto kwa uthibitisho na kuidhinishwa na uongozi wa Kanisa kisha kutuma Compassion International Tanzania na pia kutuma nakala Ofisi ya Katibu wa Dayosisi AICT Dayosisi ya Shinyanga.
xxi. Kuhakikisha kuwa taarifa zote za fedha na watoto zinatunzwa vizuri na kuhuishwa kila mara zinapohitajika.
xxii. Kuhakikisha mazingira ya Walengwa kituoni ni salama kwao kujifunza na kushiriki katika programu zote za kituo.
xxiii. Kushirikiana na watenda kazi wengine kuhamasisha upatikanaji wa raslimali za ndani kwa ajili ya miundombinu inayohitajika kwa walengwa kujifunza.
xxiv. Kufuatilia kwa karibu maendeleo ya kiroho, kiafya, kielimu na kijamii ya mlengwa mmoja aliye katika programu.
xxv. Atawajibika kwa matokeo tarajiwa ya walengwa, viashiria vya utendaji na matokeo ya ukaguzi, kwa mujibu wa kanuni za fedha za AICT na miongozo mingine ya fedha iliyokubaliwa.
xxvi. Kuhakikisha kuwa taarifa zote za watoto na Kanisa zilizoko katika mfumo wa taarifa wa Compassion connect ni sahihi na zimehuishwa.
xxvii. Kuhakikisha zawadi zilizotumwa na wafadhili zinawafikia walengwa kwa wakati na kwa asilimia mia moja.
xxviii. Kushiriki katika mafunzo yanayoandaliwa kwa ajili ya huduma ya mtoto na vijana.
xxix. Kuhakikisha watoto walioandikishwa katika Kituo kwa ajili ya ufadhili ni wale tu wanaokidhi vigezo vilivyowekwa katika Ushirika-wenza.
xxx. Kushiriki kikamilifu ibada za kila siku asubuhi pamoja na watendakazi wote kabla ya kuanza kazi.
xxxi. Atafanya kazi zingine zinazohusiana na kazi yake kama atakavyopangiwa na uongozi wa Kanisa.

## 3. MTENDAKAZI WA JAMII (SOCIAL WORKER) – NAFASI 01

**SIFA ZA WAOMBAJI**

i) Awe Mkristo aliyeokoka na kujitoa kwa Bwana Yesu; mwenye maisha ya Ushuhuda ya kila siku. Mwenye moyo wa kujitoa, kutumika kanisani na mpenda maendeleo, anayependa kufanya kazi na watoto na vijana kutoka katika mazingira magumu.
ii) Awe tayari kushiriki Ibada za Kanisa la AICT katika kipindi cha utumishi wake ili aweze kuwavuta walengwa waje kwa Yesu.
iii) Awe na elimu ya ngazi ya Stashahada **(Diploma)** au Shahada ya kwanza **(Digrii)** na kuendelea katika maswala ya Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii, Sosholojia, Usimamizi wa Miradi, Uongozi & Utawala, Usimamizi wa rasilimali watu.
iv) Awe na moyo wa kuwapenda watoto, na kutumika kanisani.
v) Awe na uwezo wa kuongea, kusoma, na kuandika kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili kwa ufasaha.
vi) Asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa la unyanyasaji wa mtoto.
vii) Awe na uwezo na elimu ya kutumia kompyuta hasa programu kama 'Micro-soft office' (Word, Excel, Power Point) na Email. viii. Awe na uzoefu katika uandishi na usimamizi wa miradi ya maendeleo.
viii) Awe na umri kuanzia miaka 23 na asizidi miaka 45.

**Kazi na majukumu ya Mtendakazi wa Jamii (Social Worker).**

i. Atamshuhudia Yesu Kristo kwa uaminifu na kuwa mtetezi wa watoto na vijana.
ii. Kuwatia moyo wazazi na walezi wa watoto na vijana na wajumbe wa kanisa kuwasaidia watoto na vijana kukua kiroho na kuwa na maendeleo ya mazuri kimasomo.
iii. Kuungana na watenda kazi wengine kuwa sehemu ya waalimu wa watoto/vijana siku za program .
iv. Kuandaa mpango kazi wa kila wiki na kila mwezi kisha kuiwasilisha kwa Mratibu wa Kituo.
v. Kuandaa taarifa ya utekelezaji ya wiki na ya mwezi kisha kuiwasilisha kwa Mratibu wa Kituo.
vi. Kushiriki vikao vyote halali vilivyopangwa na kituo cha Huduma ya Mtoto, Compassion Intrernational na Kanisa la AICT.
vii. Kufatilia hali za ujumla za maendeleo ya Watoto au vijana majumbani mwao mara zinapohitajika na kuchukua/kupendekeza hatua muhimu kuchukuliwa.

viii. Kuandaa ripoti ya kazi ya kila wiki,mwezi na robo na kuiwasilisha kwa mratibu.

ix. Kushirikiana na watenda kazi wengine wa Kituo, Mchungaji wa kanisa la Mtaa na Kamati ya Huduma ya Mtoto katika kutatu changamoto zote zitakazojitokeza katika utendaji kazi wa siku kwa siku.

x. Atasimamia maono ya maendeleo ya ujumla ya mtoto na kijana na amali za huduma wakati wote wa Uhai wa kituo cha Huduma ya Mtoto.

xi. Kushirikana na watenda kazi wengine kuandaa mpango kazi na bajeti ya mwaka ya kituo cha maendeleo ya mtoto na kijana na kuwasilisha kwa Kamati ya Huduma ya Mtoto kwa uthibitisho na kuidhinishwa na uongozi wa kanisa kisha kutuma Compassion International Tanzania na kutuma nakala Ofisi ya Katibu Mkuu AICT Dayosisi ya Shinyanga.

xii. Kuhakikisha kuwa taarifa zote za watoto zinatunzwa vizuri na kuhuishwa kila mara zinapohitajika.

xiii. Kuhakikisha mazingira ya Walengwa kituoni ni salama kwao kujifunza na kushiriki katika programu zote za kituo.

xiv. Kushirikiana na watenda kazi wengine kuhamasisha upatikanaji wa raslimali za ndani kwa ajili ya miundombinu inayohitajika kwa walengwa kujifunza.

xv. Kufuatilia kwa karibu maendeleo ya kiroho, kiafya, kielimu na kijamii ya mlengwa mmoja mmoja aliye katika programu.

xvi. Atawajibika kwa matokeo tarajiwa ya walengwa, viashiria vya utendaji na matokeo ya ukaguzi, kwa mujibu wa kanuni za fedha za AICT na miongozo mingine ya fedha iliyokubaliwa.

xvii. Kuhakikisha kuwa taarifa zote za watoto na Kanisa zilizoko katika mfumo wa taarifa wa Compassion connect ni sahihi na zimehuishwa.

xviii. Kuhakikisha zawadi zilizotumwa na wafadhili zinawafikia walengwa kwa wakati na kwa asilimia mia moja. xxiv. Kushiriki katika mafunzo yanayoandaliwa kwa ajili ya huduma ya mtoto na vijana.

xix. Kuhakikisha watoto walioandikishwa katika Kituo kwa ajili ya ufadhili ni wale tu wanaokidhi vigezo vilivyowekwa katika Ushirika-wenza.

xx. Awe tayari kushiriki ibada za kanisa la AICT kipindi cha utumishi wake ili aweze kuwavuta walengwa waje kwa Yesu ikiwepo ibada za kila siku asubuhi pamoja na watenda kazi wenzake kabla ya kuanza kazi.

xxi. Atafanya kazi zingine za zinazohusiana na kazi yake kama atakavyopangiwa na uongozi wa kanisa na mwajiri wake na wasimamizi wake.

**MAELEZO YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE**

I. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45 na usiopungua miaka 25.
II. Awe na Cheti cha kuzaliwa.
III. Barua ya Mchungaji wa Kanisa yenye maelezo ya ushuhuda wa Imani, ushuhuda wa kutoa Zaka na mwenendo bora. Barua iwe imetiwa sahihi na mhuri wa Kanisa analotoka.
IV. Maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika.
V. Majina ya wadhamini watatu (referees) wa kuaminika, anuani na zao namba za simu.
VI. Vyeti vya taaluma na uzoefu au vyeti vya kuhudhuria kozi.
VII. Viambatanisho vyote viwekwe Pamoja yaani PDF.
VIII. Kutokuzingatia maelekezo kutapelekea maombi yako yasipokelewe.

**NB:**

a. MWOMBAJI AWE TAYARI KUFANYA KAZI KATIKA KITUO CHOCHOTE CHA HUDUMA YA MTOTO ATAKACHOPANGIWA NA UONGOZI WA DAYOSISI.
MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI NI **TAREHE 09/05/2025 SAA SITA KAMILI USIKU.**

b. MAOMBI YOTE YATUMWE KWA BARUA PEPE (EMAIL) NA SI VINGINEVYO KWENYE KUPITIA: **aictshyrecruitment@gmail.com**
NA YA ELEKEZWE KWA;
Katibu wa Dayosisi,
Africa Inland Church Tanzania,
Dayosisi ya Shinyanga
S. L. P. 53
Shinyanga.

**IMETOLEWA NA KATIBU WA DAYOSISI AICT DAYOSISI YA SHINYANGA KWA NIABA YA BARAZA LA UTENDAJI AICT DAYOSISI YA SHINYANGA TAREHE 02/05/2025**